

Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

Mtandao umekuja wakati mwafaka kukomesha biashara ya binadamu

USAFIRISHAJI haramu wa binadamu unaowaathiri zaidi wanawake, wasichana na watoto unawasukuma wadau kuanzisha mtandao wa kupambana na biashara hiyo inayoolekea kushamiri Tanzania.

Baadhi ya walioguswa na kuunda mtandao huo ni asasi mbalimbali zikiwamo za kidini, vyo viki vyama vya kutetea abiria na vya wamiliki wa vyombo vya usafiri ambao wameungana na kupanga kutoa elimu ya kusaidia jamii kuachana na kusafirisha na kuuza binadamu wenzao.

Mtandao wa Tanzania Network Against Human Trafficking (TANAHUT), kwa mujibu wa Mwenyekiti Edwin Mugambila, unapambana kutokana na biashara hiyo kuumiza maelfu ya watu na kuwaachia athari kubwa kwenye maisha.

Anasema wahusika hasa wasichana huchukuliwa vijijini kwa ahadi za kupelekwa mijini kufanya kazi, lakini wakifikishwa badala ya kufanya kazi walizoahidiwa, zikiwamo ndani hutumikishwa kingono kwenye madanguro, hali ambayo inawaweka kwenye hatari ya kukumbwa na magonjwa ya ngono, kutumia dawa za kulevya na vileo na kushiriki uhalifu.

Kutokana na mazingira hayo, mtandao huo unajipanga kuanza kutoa elimu mwezi honi mwa mwezi huu, katika maeneo yote ya Dar es Salaam ambayo biashara hiyo ya ngono hufanyika.

Mbali na Dar es Salaam wadau wa mtandao huo wengine watakuwa jijini Dar es Salaam na kisha wataingia maeneo ya vijijini ambako wasichana na wanawake huchukuliwa na kupelekwa mijini kwa ahadi ya kupewa kazi.

Kwa mujibu wa Mugambila, elimu hiyo itatolewa kwa muda wa miaka mitano, na baada ya hapo, watafanya tathmini ya elimu hiyo, kisha matokeo ndiyo yatawapa picha halisi ya mafanikio, changamoto na walipokwama.

Muungwana naunga mkono mipango na mkakati ya mtandao huo, ili kunusuru kundi hilo dhidi ya hatari za magonjwa, dawa za kulevya, athari kisaikolojia na kuwaharibia maisha na kuvunja utu wao.

Jijini Dar es Salaam yapo baadhi ya mae-

neo ambayo biashara hiyo imekuwa ikifanyika, inawezekana baadhi ya wahusika ni wale waliotolewa vijijini kwa ahadi ya kuja jijini kufanya kazi na kujikuta wakiishia kutumikishwa kwenye biashara ya ngono na uhalifu.

Hivyo, kuwapo kwa elimu hiyo kunaweza kuwajengea uelewa wahusika na hatimaye wakaacha kuwa katika mazingira hayo hatarishi ambayo huenda baadhi yao wanadhani ni ya kawaida na kumbe ni hatari.

Kimsingi, biashara hiyo haramu ya kusafirisha binadamu hairuhusiwi, ndiyo maana wiki iliyopita, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam, iliwahukumu watu watatu kwenda jela miaka 25 baada kukutwa na hatia ya kujihusisha na jinai hiyo.

Wakati mtandao huo ukijiandaa kufanya kazi baadhi ya wahusika wakinaswa, ninad-nafasi yake kuunga mkono na kushiriki kuu-nusuru wengine wasiingizwa kwenye kadhia hiyo inayohatarisha maisha.

Si vibaya kutoa taarifa kwa polisi, uhamiaji na ustawi wa jamii, vijiji na viongozi wa mitaa iwapo mtu kwenye eneo analoishi au kufanyia kazi ataona kuna dalili za kuwapo kwa biashara hiyo ili kusaidia kundi hilo kuwa salama.

Hata huko vijijini ambako inaelezwa kuwa wasafirishaji wapo na hutoa ahadi tele za kazi na kumbe ni kutumikisha mabinti kwenye biashara ya ngono, ni vyema elimu ikatolewa zaidi kwa wazazi na walezi nao pia wakawa sehemu ya kutoa taarifa.

Inawezekana huwa wanaruhusu watoto wao kuchukuliwa kwenda mijini wakiamini kwamba, wakifika na kuanza kazi wanapata mishahara ya kuwawezesha kwa chochote.

Ninadhani kwamba, watoto, wazazi na walezi hao wakielemeshwa, watakuwa makini na watu hao wanaowafuata kwa ahadi ya kazi na kumbe lengo ni kuwatumikisha kwenye biashara ya ngono.

Hivyo, si vibaya kila mmoja kuhakikisha uhalifu huo unakomeshwa, lakini wahusika kujengewa uwezo wa kujitambua ili wawe makini na wote wanaojihusisha na biashara hiyo ambayo inaharibu utu wa mtu.